## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MEI, 2022 NA MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2022.

**Dondoo za tathmini ya Mei, 2022 na mwelekeo wa Juni, 2022:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2022 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto la chini kwa mwezi Juni, 2022 nchini.

- Katika kipindi cha mwezi Mei, mvua za Masika ambazo ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua ziliendelea kunyesha katika maeneo machache. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo machache ya pwani ya kaskazini.
- Katika mwezi Juni, 2022 hali ya joto la chini inatarajiwa kupungua hususan nyakati za usiku na asubuhi katika maeneo mengi ya nchi ikiashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe. Vipindi vya upepo mkali pia vinatarajiwa hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani na Ziwa Victoria.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2022.

Katika kipindi cha mwezi Mei, mvua za Masika ambazo ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua ziliendelea kunyesha katika maeneo machache. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo machache ya pwani ya kaskazini. Mnamo tarehe 05 Mei, 2022 kituo cha Matangatuani kilichopo kisiwani Pemba kilipima milimita 68.5 za mvua. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali pia vilijitokeza hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2022

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2022 hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani. Hali ya joto la bahari la wastani inatarajiwa katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati joto la bahari la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Aidha, hali ya joto la chini ya wastani inatarajiwa eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola na hivyo kusababisha uwepo wa upepo unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika na kusababisha Ukandamvua kuendelea kusogea kaskazini zaidi mwa nchi. Kwa upande mwingine, hali hii inatarajiwa kusababisha hewa ya ubaridi kiasi kutoka maeneo ya kusini mwa Afrika.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2022

Hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, hali ya joto la chini kidogo ya kawaida inatarajiwa katika maeneo ya miinuko hususan nyakati za usiku na asubuhi. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani na ukanda wa Ziwa Victoria. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini hususan ukanda wa pwani. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 20 hadi 26 °C kwa maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya 16 hadi 22 °C katika maeneo ya nchi kavu. Aidha, Hali ya ukavu itakayoambatana na vipindi vichache vya mvua inatarajiwa katika mwambao wa pwani hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Juni.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 hadi 14 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 10 °C. Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 hadi 20 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango vya chini ya nyuzi joto 14 °C. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 hadi 20 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu na vipindi vya upepo inatarajiwa kujitokeza.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 6 hadi 14 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya miinuko pamoja na mkoa wa Njombe yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 6 °C. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 hadi 22 °C katika maeneo mengi. Aidha, Hali ya ukavu itakayoambatana na vipindi vichache vya mvua inatarajiwa katika mwambao wa pwani hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Juni.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 hadi 14 °C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 °C katika kipindi cha mwezi Juni, 2022. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JULAI, 2022

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hali ya ukavu na baridi itakayoambatana pamoja na vipindi vya upepo mkali inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.4 USHAURI

Hali ya ukavu na upepo inaweza kuongeza upotevu wa maji kwa njia ya mvukizo na kuathiri upatikanaji wa maji kwa mazao, mifugo na matumizi mengine. Hivyo, Jamii inashauriwa kuchukua hatua za tahadhari ikiwa ni pamoja na kuzingatia matumizi mazuri ya maji na kujikinga ili kupunguza athari mbaya zinazoweza kusababishwa na hali ya hewa inayotarajiwa.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Juni, 2022 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz